



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA



Anwani : "TFS"

S.L.P. 40832

Simu Na. : (+255) (022) 2864249

DAR ES SALAAM

Nukushi : (+255) (022) 2864257

Barua Pepe: [mpingo@tfs.go.tz](mailto:mpingo@tfs.go.tz)

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb. Na. TFS AB.3/233/01**

**08 May, 2020**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MAFUNDI UJENZI (LOCAL FUNDI) – UKARABATI WA  
VYOO NA MAJIKO KWENYE JENGO LA WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA  
(TFS) –MPINGO HOUSE**

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unakusudia kufanya ukarabati wa jengo la Mpingo House lenye ghorofa 5 linalotumika kama ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - Makao Makuu. Ukarabati huo utafanyika kwenye maeneo ya vyoo pamoja na majiko. Aidha kazi zitakazofanyika ni kubadilisha mifumo ya maji safi na taka, kubadilisha *sanitary appliances* k.v urinals, masinki ya vyoo na masinki ya kunawia mikono , kuweka marumaru kwenye sakafu na kuta, kutengeneza na kufunga milango, kupaka rangi, kufunga dari (suspended ceiling), kazi za umeme, kufunga *mabble stone* kwenye majiko na sehemu za kunawa mikono na kukarabati bomba za Viyoyozi (AC) zinazovuja.

Ukarabati huu utatekelezwa kwa kutumia mwongozo wa **FORCE ACCOUNT** kwa usimamizi wa wataalam wetu wa ndani.

Hivyo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi tajwa hapo juu katika fani, sifa na masharti kama yalivyoainishwa katika tangazo hili kuomba kazi katika fani zifuatazo;

## **FANI, SIFA NA MASHARTI ZA MAFUNDI ZINAZOHITAJIKA;**

### **A. FUNDI UASHI NA RANGI**

1. Awe na uwezo wa kujenga marumaru kwenye kuta na sakafu (floor and wall tiles).
2. Awe na timu ya kutosha ya mafundi wasaidizi na vibarua wenye weredi wa kazi.
3. Awe na uwezo wa kupaka rangi kwenye kuta.

### **B. FUNDI UMEME**

1. Awe na uzoefu wa kufunga umeme kwenye majengo ya Serikali.
2. Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na kazi hii yenye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tsh. 10,000,000 (milioni kumi).
3. Lazima aambatanishe mkataba wa kazi wenye thamani tajwa hapo juu kutoka kwa mwajiri aliyempa kazi hiyo.
4. Awe amesajiliwa na kupata Leseni kutoka Ewura.
5. Awe na uwezo wa kufunga vifaa vya kung'amua moto (fire detectors).

### **C. FUNDI BOMBA**

1. Awe na uwezo wa kutengeneza mfumo wa maji taka uliokamilika utakaojumuisha *insection chambers*.
2. Awe na uwezo wa kutengeneza mfumo wa maji safi uliokamilika.
3. Awe na uwezo wa kufanya kazi za bomba kwenye majengo marefu.

### **D. FUNDI SEREMALA**

1. Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya aina mbalimbali pamoja na kuifunga.
2. Awe na uwezo wa kufunga vitasa na kufanya *finishing* vizuri kwenye milango hiyo.

### **E. FUNDI WA KUFUNGA MABBLE STONE**

1. Awe na uwezo wa kufunga mabble stone kwenye majiko na sehemu za kunawa mikono na kufanya finishing vizuri kwenye maeneo hayo.

#### **F. FUNDI WA DARI (SUSPENDED CEILINGS)**

1. Awe na uwezo wa kufunga dari (suspended ceiling) kwenye majengo ya serikali.
2. Awe na uwezo wa kufanya kazi akishirikiana na mafundi wengine k.v fundi umeme, bomba n.k.

#### **G. FUNDI WA AC (VIYOYOZI)**

1. Awe na uwezo wa kurekebisha bomba za AC zinazovuja.
2. Awe na uwezo wa kufanya kazi akishirikiana na mafundi wengine k.v fundi umeme, bomba, dari n.k.

#### **MASHARTI YA UJUMLA KWA WAOMBAJI**

1. Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania.
2. Mwombaji lazima awe na akaunti ya benki iliyo hai.
3. Mwombaji lazima aandike barua ya maombi akiambatanisha nyaraka zote kama zilivyotajwa katika tangazo hili, hii ni pamoja na picha ndogo (passport size) mbili za rangi.
4. Fundi atatakiwa kuomba kazi moja tu na sio zaidi.
5. Mafundi wenye sifa hizo watatakiwa kufika ofisi ya Wakala wa Huduma za Misisitu Tanzania ghorofa ya 2 chumba Na. 206 ili kuziona kazi zinazotakiwa kufanyika kabla ya kuandika barua ya maombi hayo. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/05/2020 saa 8:00 mchana .
6. Cheti ni sifa ya ziada kwa mwombaji.
7. Mwombaji lazima aambatishe barua ya mdhamini na barua kutoka Ofisi ya Serikali ya Kijiji / Mtaa.
8. Fundi atakayepata kazi lazima apatikane / awepo muda wote eneo la kazi.

9. Barua za maombi yote ziwasilishwe kwa njia ya mkono kwenye ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – Mpingo House ghorofa Na. 2 chumba Na. 206 zikiwa zimeandikwa anwani ifuatayo; **Mtendaji Mkuu, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, S.L.P 40832, NYERERE ROAD, DAR ES SALAAM.**

MTENDAJI MKUU,  
Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania,  
P.O.BOX 40832,  
**DAR ES SALAAM.**